

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA

Telegram "AFYA", **DODOMA**
Namba ya Simu: +255 26 2323267
Nukushi No: +255 22 2138060
Barua zote zitumwe kwa **Katibu**
Mkuu



Mji wa Serikali – Mtumba,
Barabara ya Afya,
S.L.P 743
40478, DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

**KUHUSU UGONJWA WA MPOX KATIKA NCHI ZINAZOPAKANA
NA TANZANIA**

Dodoma, 03 Agosti, 2024.

Wizara ya Afya inajukumu la kufuatillia na kutolea taarifa za mwenendo wa magonjwa hususani yale ya milipuko pamoja na tetesi za magonjwa ndani na nje ya nchi.

Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO), kumekuwa na taarifa za uwepo wa Ugonjwa wa Mpox (*awali ukijulikana kama Homa ya Nyani*) katika nchi mbalimbali duniani unaosababishwa na Virusi vya Mpox. Kuanzia Mei 2022 ugonjwa huu ulipoanza hadi kufikia tarehe 31 Mei 2024, wagonjwa 97,745 na vifo 203 vimetolewa taarifa kutoka nchi 116 duniani. Hata hivyo, kwa siku za hivi karibuni kumekuwepo taarifa za ongezeko la wagonjwa na vifo katika baadhi ya nchi za jirani kama Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. **Wizara ya Afya inautaarifu umma kuwa mpaka sasa Tanzania ni salama na hakuna mgonjwa yoyote aliyepatikana na ugonjwa huo.**

Ugonjwa wa Mpox unaweza kusambaa kutoka kwa mtu mwenye maambukizi kwenda kwa mwingine kwa njia zifuatazo; kupitia maji maji ya mwili ikiwemo mate, matapishi, jasho, mkojo; matone ya mfumo wa njia ya hewa; ngozi kupitia kugusana na kujamiana na mtu mwenye maambukizi; ama kutumia vifaa, matandiko au kugusa sehemu zilizo na vimelea vya ugonjwa huu. Aidha, ugonjwa huu unaweza pia kuenezwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Dalili kuu ya Mpox ni upele, malengelenge au vidonda kwenye mwili hasa mikononi na miguuni, kifuani, usoni na wakati mwingine sehemu za siri. Dalili nyingine ni homa, maumivu ya kichwa, misuli, mgongo, uchovu na kuvimba mitoki.

Ugonjwa huu haujaingia nchini, hivyo, ni vyema tukashirikiana kuhakikisha nchi yetu inabaki kuwa salama. Wizara inatoa tahadhari kwa Wananchi wote kuchukua hatua za kujikinga na ugonjwa wa huu kwa kutekeleza yafuatayo;-

- i. Kutoa taarifa kupitia namba **199** bila malipo endapo utamuona mtu mwenye dalili za Mpox.
- ii. Kuepuka kugusa majimaji ya mwili au ngozi ya mtu mwenye dalili za ugonjwa


wa Mpox.

- iii. Kuepuka kusalimiana kwa kupeana mikono, kukumbatiana na kubusiana mtu mwenye dalili za Mpox.
- iv. Kuepuka kugusana na mtu yejote mwenye dalili za ugonjwa wa Mpox.
- v. Kunawa mikono kila mara kwa maji tiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono.
- vi. Epuka kula au kugusa mizoga au wanyama mfano nyani au swala wa msituni.
- vii. Safisha na kutakasa vyombo vilivyotumika na mhisiba au mganjwa pamoja na maeneo yote yanayoguswa mara kwa mara.
- viii. Kuvalaa barakoa iwapo itabidi kukaa na kuongea kwa karibu na mtu mwenye dalili za Mpox.
- ix. Kuvalaa katika vituo vya huduma za afya unapoona dalili za ugonjwa wa Mpox.
- x. Watoa huduma za afya kuzingatia miongozo ya kuzuia kusambaa kwa maambukizi (IPC) wakati wote wanapowahudumia wagonjwa.

Wizara imeimarisha ufuatiliaji wa magonjwa (disease surveillance) hasa vituo vya kusimamia afya mipakani na kuhakikisha vifaa tiba na kinga viro maeneo ya kutolea huduma. Wataalamu wa afya kwenye maeneo yenye hatari zaidi wanaendelea kupatiwa mafunzo ya kutambua, kutoa huduma pamoja kujikinga. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuchukua hatua na kujikinga dhidi ya ugonjwa huu.

Wizara itaendelea kuimarisha udhibiti wa ugonjwa huo katika mipaka yote ili kudhibiti Ugonjwa usiingie nchini sambamba na kuimarisha ufuatiliaji wa wagonjwa. Hata hivyo Wizara imejipanga vyema kuhakikisha itatoa huduma bora za matibabu endapo mganjwa mwenye Mpox atagundulika kuwepo nchini Tanzania.

Imetolewa na:



Englibert Kayombo

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI**